# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# BUNGE LA TANZANIA

## ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI

**05 JUNI, 2025**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA KUMI NA TISA

## KIKAO CHA AROBAINI - TAREHE 05 JUNI, 2025

**I. DUA:**

**II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

**MWANASHERIA MKUU WA SERIKALI:**

Maelezo ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025].*

**MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA, KATIBA NA SHERIA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala, Katiba na Sheria kuhusu Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 [*The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025*].

## III. MASWALI KWA WAZIRI MKUU:

## IV. MASWALI YA KAWAIDA:

### OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

**512 MHESHIMIWA MARY FRANCIS MASANJA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itakipandisha hadhi Kituo cha Afya Buzuruga kuwa Hospitali.

**513 MHESHIMIWA FESTO RICHARD SANGA (MAKETE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, lini Serikali itaanza ujenzi wa Kituo cha Afya Matamba - Makete.

**514 MHESHIMIWA SEBASTIAN SIMON KAPUFI (MPANDA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, kwa nini majengo ya Halmashauri ya Tanganyika yaliyopo Manispaa ya Mpanda yasikabidhiwe kwa Halmashauri ya Manispaa Mpanda.

**WIZARA YA NISHATI:**

**515 MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kuna mkakati gani kuwaandaa Wananchi kutoka kwenye nishati ya kupikia waliyoizoea kuingia kwenye nishati safi ya kupikia.

**516 MHESHIMIWA SEIF KHAMIS SAID GULAMALI (MANONGA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, kwa nini Serikali inatoza gharama kubwa za kuvuta umeme Vijiji vya Chomachankola, Simbo, Nkinga, Ziba na Iborogero – Manonga.

**WIZARA YA KILIMO:**

**517 MHESHIMIWA ASHA ABDULLAH JUMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha maji kwa ajili ya umwagiliaji yanafika mashambani bila upotevu.

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

**518 MHESHIMIWA ALLY YAHYA MHATA (NANYUMBU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Chuo cha VETA Wilayani Nanyumbu.

**WIZARA YA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI:**

**519 MHESHIMIWA FELISTA DEOGRATIUS NJAU (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari:-

Je, lini Serikali itajenga mnara wa mawasiliano katika Kata ya Shimbwe ambapo hakuna mawasiliano.

**WIZARA YA UJENZI:**

**520 MHESHIMIWA SILYVESTRY FRANCIS KOKA (KIBAHA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-

Je, lini ujenzi wa kiwango cha lami wa Barabara ya Makofia - Mlandizi - Vikumburu utaanza.

## V. MISWADA YA SHERIA YA SERIKALI:

***(Kusomwa Mara ya Pili, Kamati ya Bunge Zima na Kusomwa Mara ya Tatu)***

Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2025 *[The Written Laws (Miscellaneous Amendments) Bill, 2025].*

**DODOMA** **BARAKA I. LEONARD**
**05 JUNI, 2025** **KATIBU WA BUNGE**